# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI



# JARIDA MAALUM ARUSHA


BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Mwenyekiti

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAANDISHI**
Munir Shemweta
Eliafile Solla
Hassan Mabuye
Magreth Lyimo



Mji wa Serikali Mtumba, S. L. P. 2908 | 40477- DODOMA | Simu: +255 262 963309/13/14 | Nukushi: +255 262 963316
Barua pepe: ps@lands.go.tz | Tovuti: www.lands.go.tz



*Waziri wa Ardhi Mhe. William Lukuvi akizungumza na Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru mkoani Arusha wakati wa ziara yake mkoani Arusha.*

# WAZIRI LUKUVI AFUTA WARAKA UNAOKATAZA MADIWANI KUIDHINISHA MIPANGO YA UENDELEZAJI MIJI

**Na Munir Shemweta**

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi amefuta waraka namba moja unaowaondoa madiwani kushiriki katika shughuli za uidhinishaji mipango ya uendelezaji miji katika halmashauri zao uliotolewa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi nchini.

Kabla ya kutolewa waraka huo mpya Madiwani kupitia kamati zao za mipango miji walikuwa ndiyo wenye mamlaka ya kubariki mipango ya uendelezaji miji kwenye halmashauri kupitia vikao vyao vya robo mwaka na waraka mpya unataka shughuli hizo sasa kufanywa na wataalamu wa mipango miji kwa kushirikisha sekta mbalimbali kama vile sekta za maji, barabara na umeme.

Lukuvi alifanya maamuzi hayo hivi karibuni katika ukumbi wa halmashauri ya wilaya ya Meru wakati akizingumza na madiwani wa halmashauri hiyo akiwa katika ziara ya kusikiliza na kuitafutia ufumbuzi kero za ardhi katika mkoa wa Arusha.

Alisema, kwa sasa waraka huo ameufuta mpaka utakapotolewa mwingine wenye maelekezo yatakayokuwa na tija na kusisitiza kuwa, haiwezekani kuwaondoa madiwani kupitisha mipango ya uendelezaji miji kwenye halmashauri zake kwa kuwa mamlaka ya upangaji bado ziko chini halmashauri.

"Nimeamua kuufuta waraka namba moja unaokataza madiwani kupanga mipango ya uendelezaji miji katika halmashauri zenu, huwezi kuwa na halmashauri inayoshindwa kupitisha au kubariki mipango ya wilaya katika matumizi ya ardhi" alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, wataalam wa mipango miji katika ofisi za ardhi za mikoa waendelee kuwa washauri kwa kamati za mipango miji katika mabaraza ya madiwani.

"kama vibali vya ujenzi tuliwaondolea na kupanga pia tuwaondoe, mtafanya kazi gani? hiyo haiwezekani, kwa sasa muongozo unaokuja kamati za madiwani zitapatiwa ufafanuzi wa namna bora ya matumizi ya ardhi na baadaye kupelekwa kwa maafisa mipango miji.

# RAIS SAMIA AFUTA SHAMBA LA VALESKA ARUSHA



*Waziri wa Ardhi Mhe. William Lukuvi akisisitiza jambo wakati akielezea uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kufuta shamba la Valeska lilipo katika halmashauri ya Meru mkoani Arusha.*

## Na Munir Shemweta

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amufuta shamba la Valeska lenye ukubwa wa ekari 4,087 lililopo katika halmashauri ya wilaya ya Meru mkoani Arusha.

Uamuzi huo ulitangazwa hivi karibuni jijini Arusha na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi wakati wa ziara yake mkoani Arusha kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero za katika mkoa huo.

Uamuzi wa kufutwa kwa shamba hilo na Mhe Rais Samia Suluhu Hassan unatokana na mmiliki wake kukiuka masharti ya uendelezaji yaliyosababisha Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwasilisha mapendekezo ya kufutwa kwa mujibu wa sheria.

Moja ya masharti ya umiliki wa mashamba ni mmiliki kutakiwa kendeleza moja ya nane ya shamba analomiliki na asipofanya hivyo hupelekewa notisi ya kufutwa na Afisa Ardhi katika eneo husika na baadaye Waziri mwenye dhamana huwasilisha mapendekezo kwa Mhe Rais kwa utekelezaji.

Hata hivyo, Waziri Lukuvi alisema halmashauri ya wilaya ya Meru itawajibika kulipa fidia kwenye maeneo yanayohitaji fidia ambapo kwa mara ya mwisho fidia ya shamba katika eneo hilo ilikuwa milioni Shilingi milioni 394.10.

Waziri Lukuvi alianisha matumizi ya shamba lililofutwa la Valeska kuwa ni ekari 1,500 kugawiwa kwa vijiji vitatu vya Kwaugoro, Valeska na Maloloni na kuongeza kuwa ekari 1,028 zitatumika kwa shughuli za kilimo huku ekari 1559 ikibaki kwa matumizi mbalimbali kama vile makazi na biashara

*Waziri wa Ardhi Mhe. William Lukuvi akimsikiliza Bibi aliyemkuta ofisi ya Mkuu wa mkoa wa Arusha wakati wa ziara ya kusikiliza kero za ardhi.*






*Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Arusha Leo Komba akielezea mafanikio ya Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Arusha tangu kuanzishwa Machi, 2021.*

# KASI YA UPIMAJI ARDHI ARUSHA YAONGEZEKA

**Na Munir Shemweta**

Ofisi ya Ardhi mkoa wa Arusha imeongeza kasi ya upimaji ardhi katika maeneo mbalimbali katika kipindi cha mwaka mmoja toka kuanzishwa ofisi hiyo.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Arusha Leo Komba wakati akizungumzia mafanikio ya Ofisi yake tangu kuanza rasmi kazi Mei 2020.

Alisema, ongezeo hilo la upimaji ardhi limetokana na kasi kubwa inayofanywa na ofisi yake kwa kushirikiana na ofisi za ardhi kwenye halmashauri za wilaya na miji za mkoa huo ambapo takwimu zake zinaonesha ongezeko hilo ni mara mbili ukilinganisha na mwaka uliopita.

Kwa mujibu wa Komba, wakati ofisi yake ilipozinduliwa upimaji ardhi kwa mkoa mzima ulikuwa viwanja 41,000 lakini hadi kufikia Mei 2021 mkoa huo umepima viwanja 81,215 ambapo kati ya viwanja hivyo 33,057 ni vya urasimishaji makazi holela.

''Baada ya ongezeko hilo la upimaji kasi ya uandaaji hati nayo imeongezeka ambapo kazi iliyopo mbele yetu ni kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchukua hati za ardhi kwa kuwa mwananchi atakapopata hati atakuwa ameongeza thamani ya ardhi yake'' alisema Komba.

Akielezea kero za ardhi katika mkoa wa Arusha, Komba alisema kasi ya kutatua kero za wananchi kwa sasa imekuwa rahisi kwa kuwa ofisi hiyo inaweza kufanya ziara za kushtukiza kwenye maeneo mbalimbali tofauti na wakati mkoa huo ulipokuwa chini ya ofisi ya kanda ya kaskazini.

''Kazi ya kushughulikia kero za wananchi sasa ni rahisi na hivi karibuni tu tuliweza kutatua changamoto ya mama mlemavu wa macho aliyemtaja kwa jina la Bertha Solomon anayeishi kijiji cha Ngaramtoni ambaye ilikuwa vigumu kwake kulipia hati yake ya ardhi lakini chini ya usimamizi wangu suala hilo tuliweza kulitatua kwa haraka na mwenyewe aifurahi sana'' alisema Komba.

Hata hivyo, Kamishna Komba alisema, changamoto kubwa kwenye mkoa wake ni kupanuka kwa kasi kwa mji wa Arusha kunakosababisha wananchi kununua maeneo na kujenga bila kuzingatia mipango miji na kueleza kuwa, kwa sasa mkoa huo una mazoezi ya Urasimishaji na lile Kutambua Vipande vya Ardhi kwenye maeneo ya makazi holela ambapo wamiliki wake wanapatiwa leseni za makazi.



*Bertha Solomon ambaye ni mlemavu wa macho mkazi wa Ngaramtoni Arusha akielezea namna alivyosaidiwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Arusha kupata hati ya ardhi.*

# MIAMALA YA NYARAKA MPAKA ILIPIWE KODI YA ARDHI ARUSHA

**Na Munir Shemweta**

Msajili wa Hati na Nyaraka Msaidizi ofisi ya ardhi mkoa wa Arusha Juliana Ngonyani amesema Ofisi yake imejiwekea utaratibu wa kutopitisha nyaraka kwa ajili ya kufanya muamala wowote bila kulipiwa kodi ya pango la ardhi.

Hatua hiyo inalenga kuhakikisha miamala yote inayofanyika katika ofisi ya Msajili wa Hati na Nyaraka inalipiwa kodi ya pango la ardhi na hivyo kuiwezesha serikali kukusanya mapato yake kupitia kodi ya pango la ardhi.


Akizungumza hivi karibuni mkoani Arusha, Ngonyani alisema mwananchi anatakiwa kuhakikisha amelipa kodi ya pango la ardhi kabla ya kuwasilisha muamala kwa ajili ya usajili na kubainisha kuwa hatua hiyo imewezesha mkoa huo kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato ya kodi ya ardhi ukilinganisha na mika iliyopita. ''Ofisi ya Ardhi mkoa haipitishi muamala wowote kama vile usajili wa mkopo (mortage), uhamisho wa miliki (transfer) kama mhusika hajalipa kodi ya pango la ardhi na kwa mtindo huu tumewezesha mapato kupanda'' alisema Ngonyani.

Kwa mujibu wa Ngonyani, ofisi ya Ardhi mkoa wa Arusha tangu kuzinduliwa kuanza kazi imeshasajili miala 5,745 ya nyaraka mbalimbali pamoja na kusajili hati 1,562 za ardhi na kuweka wazi kuwa matarajio ya ofisi hiyo ni kuongezeka kwa usaji wa nyaraka mbalimbali.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanasajili nyaraka sambamba na kutumia ofisi hiyo kujiridhisha uhalali wa miliki za ardhi ili kuepuka utapeli au hati bandia.

Aidha, katika kuondoa usumbufu kwenda kuchukua hati za ardhi katika Ofisi ya Msajili wa Hati na Nyaraka mkoa, Msajili huyo wa Hati Msaidizi alisema ofisi yake imekuwa ikipelekea hati za kwa wamiliki kwenye halmashauri na kutolea mfano kuwa tayari walishapeleka hati kwenye wilaya za Longido Hati 45, Monduli 86, Karatu Hati 38 na kwa zile halmashauri zilozoko mijini walibandika majina ya wamiliki wake katika mbao za matangazo za ofisi hizo.

Hata hivyo, aliongeza kuwa, ofisi yake imekuwa karibu na wananchi kwa kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusiana na huduma za ofisi yake na kusisitiza kuwa lengo ni kuhakikisha wananchi wanazielewa huduma hizo tofauti na dhana iliyojengeka kuwa huduma inayotolewa ni ya kutoa hati.




*Msajili wa Hati na Nyaraka Msaidizi mkoa wa Arusha Juliana Ngonyani akizungumzia mikakati ya ofisi yake.*

# MIPANGO YA UENDELEZAJI MIJI KUZINGATIA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA

**Na Munir Shemweta**



Ofisi ya Mipango Miji katika Ofisi ya Ardhi mkoa wa Arusha imeweka sharti la mipango yote ya uendelezaji miji katika jiji la Arusha upitishwaji wake lazima uzingatie Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Afisa Mipango Miji mkoa wa Arusha Shaiyo Chuma wakati akizingumzia mikakati ya ofisi yake tangu kuanzishwa Ofisi ya Ardhi mkoa wa Arusha.

Chuma alisema, katika kipindi cha mwaka mmoja tangu kuanzishwa ofisi ya ardhi mkoa wa Arusha pamoja na mambo mengine ofisi hiyo inasimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe Jiji la Arusha unaohusisha wilaya za Arusha na Arumeru.

''Mipango yote ya uendelezaji miji katika jiji la Arusha ambayo haitazingatia Mpango Kabambe wa jiji la Arusha tutakataa kuiidhinisha, hatutakubali kuidhinisha mpango unaoenda tofauti na mpango kababmbe' alisema Chuma.

Kwa mujibu wa Afisa mipango miji wa mkoa wa Arusha, tangu Tanzania ipate uhuru mkoa wa Arusha umeidhinisha takriban mipango 318,860 huku zoezi la urasimishaji likizalisha jumla ya viwanja 100,444 vilivyopimwa na makampuni binafsi pamoja na serikali kupitia ofisi zake za ardhi.

changamoto mbalimbali kutoka kwa wamiliki kuhamisha alama za miaka kwa kisingizo cha mahali ilipowekwa hapakuwa sahihi na kuongeza kuwa halmashauri zimekuwa zikiendelea na maziezi ya urasimishaji katika Lemala, Kisyeri na karatu na kuongeza kuwa kasi kubwa sasa imeelekezwa katika upimaji na umilikishaji.



# HALMASHAURI SITA ARUSHA ZASHINDWA KUAINISHA MAENEO YA UMMA YANAYOHITAJI KUPIMWA

**Na Munir Shemweta**




*Mpima Mkuu wa Ofisi ya Ardhi mkoa wa Arusha Romanus Sanga akielezea mikakati ya upimaji ardhi katika mkoa wake*

Imebainika kuwa jumla ya halmashuri sita kati ya saba za mkoa wa Arusha zimeshindwa kuainisha maeneo ya umma yanayohitaji kupimwa na kumilikishwa ardhi kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza hivi karibuni mkoani Arusha, Mpima Mkuu katika Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Arusha Romanusi Sanga alisema, mkoa wa Arusha wenye ukubwa wa ardhi mita za mraba 34,526 umepima jumla ya maeneo 81,215 na 2,696 ni mashamba.

Alibainisha kuwa, katika kuhakikisha ardhi ya mkoa huo inapimwa na wamiliki wake kumilikishwa ofisi ya Ardhi mkoa wa Arusha ilizitaka halamasahauri katika mkoa huo kuanisha maeneo ya umma ili yaweze kupimwa na Taasisi zake kumilikishwa,.

Hata hivyo, Mpima huyo Mkuu wa Mkoa wa Arusha alisema, kati ya halmashauri saba zilizopelekewa maombi ni halmashauri moja tu ya Ngorongoro ndiyo iliyoanisha na kuwasilisha kupimiwa maeneo yake ya umma. Aliyataja maeneo ya umma yaliyopimwa katika wilaya hiyo kuwa ni Hospitali ya Wilaya, Chuo cha Ualimu, Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), shule mbili za msingi pamoja na shule ya Sekondari ya Semunge.

Kwa mujibu wa Sanga, halmashauri ambazo hazijaitikia wito wa kuanisha maeneo ya umma kuwa ni Longido, Jiji la Arusha, Halmashauri ya Arusha DC, Meru, Monduli pamoja na Halmashauri ya Karatu ambapo amezikumbusha kuainisha haraka maeneo yake ili ziweze kufanyiwa upimaji na kuondoa uamixi na migogoro inayoweza kutokea.